SHUGHULI ZA KISWAHILI - GRADE 3
2023 END TERM 1 EXAMS

SEHEMU YA 1:
KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA
<u>Mwalimu atamwuliza mwanafunzi maswali yafuatayo, mwanafunzi ayajibu vilivyo</u>

1. Mzazi wa kike ni?
   (Mwanafunzi ajibu)
2. Mama wa baba ni?
   (Mwanafunzi ajibu)
3. Baba wa mama ni?
   (Mwanafunzi ajibu)
4. Mwalimu hufunza akina nani?
   (Mwanafunzi ajibu)
5. Mimi nina umri wa miaka?
   (Mwanafunzi ajibu)

SEHEMU YA 2:
KUSOMA KWA SAUTI
<u>Soma hadithi hii kwa sauti</u>
Lochita aliishi na wazazi wake Betei. Wazazi hao walimpenda sana. Wakati wa likizo, Lochita aliwatembelea shangazi na mjomba. Aliwanunulia binamu zake kalamu na vifutio.
Shangazi alimwambia Lochita abaki ili watembelee mbuga ya wanyama. Mbugani waliwaona wanyama wengi, waliwaona simba, ndovu na chui. Lochita alipiga picha ili awaonyeshe wazazi wake.

SEHEMU YA B:
SEHEMU Ya 1: KUSOMA UFAHAMU
<u>Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali</u>
Ilikuwa ni siku ya Alhamisi, kulikuwa na mashindano ya kuimba nyimbo. Wanafunzi wa shule jirani walikuja shuleni kwetu. Tulienda kwenye gwaride. Bendera ilipandishwa tuliimba wimbo wa taifa, Baadaye tuliingia ukumbini. Gredi ya tatu iliimba vizuri. Tulipewa zawadi. Grace alikariri shairi. Naye pia alipokea zawadi.